TANGAZO LA SERIKALI Na. 1026 La Tarehe 11/12/2020

(SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA. 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya kifungu 153)*

## SHERIA NDOGO ZA UVUNAJI WA MAJI YA MVUA ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA ZA MWAKA,2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Uvunaji wa Maji ya Mvua za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama za Mwaka 2020.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Mhandisi wa maji pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"uvunaji wa maji ya mvua" maana yake ni kukusanya na kutunza maji ya mvua kutoka kwenye ardhi, miamba au kutoka kwenye paa la nyumba kwa kutumia teknolojia rahisi ya makinga maji.

Uvunaji wa maji ya mvua

4. Kila mtu katika eneo la Halmashauri atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa aanajenga miundo mbinu ya kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi katika vyombo maalum.

.

Uidhinishaji wa Michoro ya ujenzi wa nyumba

5.-(1) Bila kuathiri masharti ya Sheria nyingine, Halmashauri haitaidhinisha michoro ya ujenzi wa nyumba endapo michoro hiyo haitaonyesha miundombinu ya kuvunia maji ya mvua

(2) Kila mmiliki wa jengo lililopo katika eneo la Halmashauri ambalo yalijengwa kabla ya kutungwa kwa Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa anajenga vyombo vya kuvuna na kuhifadhia maji ya mvua.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

6.- (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote kukagua ujenzi wa miundo mbinu ya kuvunia maji ya mvua pamoja na vyombo vya kuhifadhia maji hayo.

(2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuzuia kuendelea kwa ujenzi katika hatua yoyote ya ujenzi endapo atagundua kuwa nyumba inayojengwa haikuwekewa miundo mbinu ya kuvuna maji ya mvua.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayejenga miundo mbinu ya kuvunia maji ya mvua kuhakikisha kwamba anafuata viwango vitakavyoelekezwa na Afisa Mwidhiniwa.

Makosa na adhabu

7.-(1) Mtu atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atakataa au atashindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Afisa Mwidhiniwa kuhusu utekelezaji wa masharti ya Sheria Ndogo hizi;

(b) atajenga au kuanza ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua bila kupata kibali cha Halmashauri;

(c) atajenga jengo ambalo mchoro

wake hauonyeshi miundombinu ya kuvuna maji ya mvua na haukuidhinishwa na Halmashauri; au

(d) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufililisha kosa

8. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi

______

JEDWALI

______

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 8*)

HATI YA KUFILILISHA KOSA

Mimi…………………………….nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, kwamba tarehe ………mwezi………..mwaka……….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha……………….cha Sheria Ndogo za Uvunaji wa Maji ya Mvua za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama za mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa shilingi laki mbili na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………………………………..ya Mwezi………………….Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo…………………………………….
Saini………………………………………Tarehe……………………………………

*Tangazo la Serikali Na. 1026 (Linaendelea.)*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa baraza la Madiwani wa Halmashauri uliopitishwa na kufanyika tarehe 24/2/2017 mbele ya:-

ENG. GODFREY T. SANGA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mkalama*

JAMES J. MKWEGA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mkalama*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Novemba, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.)
*WN-OR-TAMISEMI*